# AckySHINE.com

# Umri unaofaa kuoa

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Kuoana maana yake ni kuwajibika kwa maisha yako na mke au mume wako. Mara nyingi kuoana kunaambatana na kuzaa watoto. Ni vigumu sana kutambua umri sahihi wa mtu kuoa au kuolewa, kwa sababu watu wanatofautiana katika kuamua ni lini yuko tayari kujitegemea na kuwajibika kumtunza mtu mwingine. Wengine wanakuwa tayari katika umri wa miaka 20 na wengine katika umri mkubwa zaidi.

Kwa vile kuoa au kuolewa mara nyingi kunahusishwa na mtu kuwa mzazi, kuna vipengele vya kiafya vinavyofaa kuzingatia. Kwa mfano siyo vema msichana kuzaa kabla hajafikisha umri wa miaka 18, kwa sababu mwili wake hauko tayari kuzaa mtoto. Nyonga i nakuwa bado ni nyembamba, viungo vya uzazi ni vidogo na havijakomaa kiasi ambacho vinaweza kuharibika wakati wa kuzaa mtoto. Kwa hiyo basi unashauriwa kusubiri i kuoana mpaka hapo utakapokuwa umejenga msingi i mzuri i wa maisha yako. Kabla hujawa tayari kuoa au kuolewa unaweza kuwa na urafiki na yule aliye mtarajiwa wake ili taratibu muweze kuelewana tabia, yale anayoyapenda na asiyoyapenda na kujenga msingi mzuri wa uhusiano.